

ABDULRAHMAN AL-SUMAIT UNIVERSITY (SUMAIT)



MWALIKO WA KUWASILISHA ZABUNI KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA ZA CHAKULA

ZABUNI NAMBA: SUMAIT/NCS/02/2026

06/10/2026

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha **Abdulrahman Al-Sumait (SUMAIT)** anawaalika watoa huduma za chakula wenye sifa, uwezo na uzoefu kuwasilisha nukuu za bei kwa ajili ya kutoa huduma za upishi na chakula katika Chuo Kikuu. Lengo la mwaliko huu ni kumpata mtoa huduma anayeaminika na mwenye uwezo wa kutoa chakula bora, salama, chenye kuzingatia usafi na afya na kwa bei inayokubalika kwa wanafunzi na/au Jamii ya Chuo Kikuu.

Watoa huduma wanaovutiwa wanaweza kupata taarifa zaidi pamoja na kukagua na kuchukua nyaraka za zabuni katika **Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait**, kuanzia saa **02:30 asubuhi** hadi saa **09:30 alasiri**, siku za **Jumatatu** hadi **Ijumaa**, isipokuwa siku za sikukuu za kitaifa.

Nukuu zote za bei zinapaswa kuwasilishwa katika **nakala moja (1) halisi (Original)** na **nakala (Copy) mbili (2)**, zikiwa zimejazwa kikamilifu na kuwekwa katika bahasha iliyofungwa vizuri, bahasha hiyo iandikwe: **“NUKUU YA BEI KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA ZA CHAKULA CHUO KIKUU CHA ABDULRAHMAN AL-SUMAIT.”**

Nukuu hizo zinapaswa kuwasilishwa kwa anuani ifuatayo:

Afisa Manunuzi,
Chuo Kikuu Cha Abdulrahman Al-Sumait (SUMAIT)
Chukwani – Zanzibar.

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha nukuu za bei ni **15/10/2026 saa 06:30 mchana (12:30hrs)**.

Nukuu zitafunguliwa mara tu baada ya muda wa mwisho wa uwasilishaji, katika kikao cha wazi na mbele ya wawakilishi wa wazabuni ambao watakuwa wamechagua kuhudhuria.

Nukuu zitakazowasilishwa baada ya muda uliowekwa (Late Bids), sehemu ya nukuu, nukuu zilizowasilishwa kwa njia ya kielektroniki, pamoja na nukuu ambazo hazikufunguliwa na kusomwa hadharani, hazitakubaliwa.

Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait kinahifadhi haki ya **kukubali au kukataa nukuu yoyote, zote au sehemu yake**, kwa mujibu wa taratibu na masharti ya manunuzi.



.....
Prof. Msafiri M. Mshewa

Makamo Mkuu

Chuo Kikuu Cha Abdulrahman Al-Sumait (SUMAIT)